**TAARIFA KWA UMMA**

# MAFANIKIO YA USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA USAJILI NA UTOAJI WA LESENI ZA VIWANDA KATIKA MIAKA 60 YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR

**Dar es Salaam-24 Aprili, 2024**

Sheria ya Taifa ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda Sura ya 46 na marejeo yake ya 2002 (The National Industries (Licensing and Registration) Act, Cap 46 R.E. 2002) ni sheria inayosimamiwa na kutekelezwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kwa pamoja na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar

Uanzishwaji wa Sheria ya Taifa ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda ililenga kusimamia Viwanda vya upande wa Tanzania bara pekee, kufikia Mwaka 1982 Sheria hiyo ilifanywa kuwa ya Muungano baada ya kufanyika kwa Marekebisho kwenye Katiba na kuongezwa Leseni za Viwanda na Takwimu kwenye orodha ya mambo ya Muungano

Kupitia marekebisho ya Sheria hiyo, imeleta mafanikio katika kipindi cha miaka sitini (60) ya Muungano wa Tanzania kwa Taasisi hizo kufanikisha utekelezaji wa usajili na utoaji wa Leseni za Viwanda nchini. Mafanikio hayo ni kama ifuatavyo;

i. Sheria ya Taifa ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda imeendelea kufanyiwa marekebisho makubwa na kuifanya ya kisasa zaidi yenye kuzingatia na kuendana na halisi ya ufanyaji biashara ya sasa. Mabadiliko hayo yaliyotokea ni kama ifuatavyo
   - Kuhamisha idhini ya Utoaji wa Leseni za Viwanda kutoka kwa Bodi ya Leseni za Viwanda kwenda kwa Msajili wa Viwanda,
   - Kufuta Kamati za Ushauri za Mikoa na jukumu lake la kushauri kuhusu Viwanda kuhamishiwa kwa Bodi ya Leseni za Viwanda,

   - Kuongeza Kifungu kinachoeleza kuhusu Uteuzi, idadi na taratibu za uendeshaji wa Bodi ya Leseni za Viwanda, na
   - kuboresha maana ya maneno mbalimbali yanayotumika kwenye Sheria hiyo kama vile Maana ya Kiwanda

ii. Kujengwa kwa Mfumo wa pamoja wa kielektroniki utakaotumika kutolea Leseni za Viwanda na Vyeti vya Usajili kwa pande zote mbili za Muungano ili kusaidia utekelezaji wa Sheria hiyo kimuungano na kurahisisha upatikanaji wa takwimu za Viwanda za nchi nzima.

iii. Kufanyika kwa Vikao vya pamoja vya mashirikiano baina ya pande mbili za Muungano vilivyojadili masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa Sheria hii kimuungano hususan mfumo ya kielektroniki, vilivyotoa ufumbuzi wa pamoja wa changamoto nyingi kwa manufaa ya pande zote mbili za Muungano.

iv. Kufanyika Marekebisho ya jedwali la ada, kwa kubadilisha malipo ya ada za Leseni na usajili wa Viwanda kutoka katika Dola za Kimarekani na kuwa katika Shilingi za kitanzania hivyo kupanua wigo wa urasimishaji wa Viwanda, hususan vidogo.

Imetolewa na;

**Kitengo cha Uhusiano**